# IKULU ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 022 ISSN 1821 - 8253 JULAI - DISEMBA 2015




# MV Mapinduzi II imewasili katika Bandari ya Malindi, Zanzibar







## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu**
Hassan K. Hassan

**Mhariri Msaidizi**
Ali S. Hafidh

**Waandishi**
Said J.Ameir
Rajab Y. Mkasaba
Haji M. Ussi
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Mahfoudha M. Ali
Amina M. Ameir

**Mpiga Picha**
Ramadhan O. Abdalla

**Msanifu**
Aziz I. Suwed

## UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.

Jarida hili linatolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

P.O.Box: 2422
Zanzibar - Tanzania
Phone: +255 223 081/5
Fax: 024 223 3722
Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz

# Maoni ya Mhariri

## Tumieni fursa zilizopo kukabiliana na umasikini

Fursa mbali mbali za kijamii na kiuchumi zitolewazo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni njia muhimu ya kulipatia ufumbuzi tatizo la umasikini. Kutumia vyema fursa hizo mbali mbali kutawasaidia wananchi kujiongezea kipato chao na kuondokana na umasikini.

Wapo wananchi wasiofahamu kwamba hata nchi ambazo leo hii zinahesabika kuwa ni miongoni mwa nchi tajiri, nazo zilikuwa masikini kama Zanzibar na nyengine ni zaidi ya Zanzibar.

Mataifa kama vile China, Singapore, Malaysia na nchi nyengine nyingi katika Bara la Asia, zilipitia katika hali ngumu ya maisha na ni vigumu leo hii kuamini kwamba nchi hizo zinahesabiwa kuwa ni miongoni mwa mataifa yenye uchumi mkubwa duniani.

Mafanikio ya mataifa hayo hayakupatikana kimiujiza. Dhamira ya kweli ya viongozi na wananchi katika kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kila mmoja kukubali kufanya kazi kwa bidii ndio siri kubwa ya mafanikio yao.

Dhamira ya kupambana na umasikini Tanzania na Zanzibar kwa ujumla wake, ni suala ambalo limekuwa likielezewa kwenye mipango yote mikuu ya kitaifa na kimataifa. Serikali imekuwa ikichukua juhudi za makusudi katika kuhakikisha kuwa inaondokana na tatizo hilo kwa kutoa fursa kadhaa.

Jitihada za Serikali katika kuimarisha miundo mbinu ya kiuchumi mjini na vijijini hazikuwa na lengo jengine zaidi ya kuendeleza mipango hiyo ya kuondokana na umasikini.

Ujenzi wa barabara za lami, usambazaji wa maji safi na salama, usambazaji wa huduma za umeme, ujenzi wa skuli mpya za kisasa na hospitali za kisasa mjini na vijijini Unguja na Pemba hayakuwa na maana nyengine zaidi ya kujenga jamii imara, yenye afya bora, iliyoelimika itakayokuwa na uwezo wa kufanya shughuli za uzalishaji mali bila ya usumbufu.

Kutokana na ukweli kwamba, vijiji vingi hivi sasa vimepata huduma ya umeme, maji safi na salama, barabara za uhakika, watu wengi wanao uwezo wa kuanzisha miradi yao na hasa baada ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuweka utaratibu mzuri wa kuwapatia mikopo ambayo itawawezesha kuanza miradi yao.

Jitihada hizi zimekuwa zikienda sambamba na mafunzo ya kilimo, ufugaji na ujasiriamali mambo ambayo yamekuwa yakifanyika kwenye vijiji mbali mbali kwa lengo la kuzifanya shughuli hizo kuendeshwa kisasa na kuleta tija zaidi kwa wanaoziendesha.

Suala kubwa ambalo limekuwa kikwazo cha kuondokana na umasikini kwa sasa ni namna ambavyo wananchi wenyewe watakavyoweza kukubali mabadiliko na hivyo kuachana na kufanyakazi kwa mazowea, wakiamini kuwa kazi pekee inayoweza kuwavusha kimaisha ni ajira kutoka Serikalini.

Bila ya shaka inawezekana kuwa tatizo hili likawa kubwa zaidi kuliko lile la kuanzisha miundo mbinu kwani kimaumbile binadamu anakuwa mgumu kubadilika. Kubadilisha mwenendo au tabia ya binadamu ni mchakato ambao huchukua muda mrefu na mafanikio yake huonekana kidogo kidogo huku ikizingatiwa ule msemo wa Kiswahili usemao "mazowea yanatabu na kuyakosa ni adhabu".

Hata hivyo wapo waliothubutu kubadilika na mafanikio yao yamekuwa yakionekana wazi wazi. Kwa mafano ilikuwa imezoeleka kwamba biashara ya nyanya/tungule, pilipili boga, tikitimaji, vitunguu maji na nyingi za aina hiyo zilifanywa tu huko Tanzania Bara na ama isingewezekana au ingekuwa vigumu biashara hiyo kuifanya hapa Zanzibar.

Lakini katika siku za hivi karibuni baada ya jitihada kubwa ya Serikali kutoa elimu kwa wananchi, imethibitika kwamba wazanzibari wenyewe wanao uwezo wa kuzalisha bidhaa hizo na kutosheleza soko la Zanzibar bila ya kuagiza bidhaa hizo kutoka Tanzania Bara na wapo wakulima wenye maisha bora zaidi hata kuliko wafanyakazi serikalini.

Kazi kubwa inayoikabili Serikali na wananchi kwa ujumla ni kutangaza mafanikio ya wale waliothubutu ili wengine nao waweze kutanabahi kuwa kumbe inawezekana kufanya maisha yakawa mazuri bila ya kutegemea ajira kutoka serikalini.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwa na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi wakipata maelezo kutoka kwa Nahodha wa Meli mpya ya MV - Mapinduzi II Abubakar Mzee (katikati) wakati walipofika katika chumba maalum cha mitambo ya kuendeshea meli, maelezo hayo yalitolewa katika shamra shamra za sherehe za uzinduzi wa Meli hiyo tarehe 12 Disemba 2015, katika Bandari ya Malindi Mjini Zanzibar

# MV Mapinduzi II imewasili katika Bandari ya Malindi, Zanzibar

Jumamosi ya tarehe 12 Disemba 2015, ilikuwa ni siku maalum kwa Wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba kuandika historia nyengine ambapo kwa mara nyingine tena Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba imeweza kutekeleza kwa vitendo dhamira yake ya kuimarisha miundombinu ya kiuchumi kama usafiri wa baharini.

Ni siku hii ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein alizindua rasmi meli mpya MV Mapinduzi II katika bandari ya Malindi Zanzibar.

Kila mzanzibari alipenda kuhudhuria na kujionea kwa macho yake tukio hilo la kihistoria la uzinduzi wa meli, lakini kwa kuwa halikuwa jambo rahisi, uwepo wa tekinolojia ya kisasa ya mawasiliano uliwafanya watu wengi kulishuhudia tukio hilo kupitia matangazo ya moja kwa moja ya kituo cha televisheni cha Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC).

Ni meli mpya na ya kisasa ambayo kila mwananchi angependa siku moja apate fursa ya kusafiri nayo. Ni meli yenye kila sifa ambazo abiria 1,200 wanaoweza kuingia melini humo wataipenda.

Meli hiyo ambayo ina uwezo wa kusafiri kati ya bandari ya Zanzibar hadi Pemba kwa saa 4 wakati safari ya Zanzibar hadi Dar es salaam inachukua saa 3 inayo madaraja 3, daraja la watu mashuhuri abiria 50, daraja la kwanza linalochukua abiria 350 na daraja la tatu abiria 800.

Lakini kitu kimoja muhimu katika meli hii ni teknolojia ya kisasa iliyotumika katika kuifanya kuwa ya kisasa. Inaelezwa kuwa meli hiyo imewekewa vifaa maalum vyenye uwezo wa kuituliza meli hiyo isiyumbe baharini wakati bahari inapochafuka na kusababisha mawimbi makali jambo ambalo linaepusha madhara kwa abiria wanaosafiri.

Aidha, meli hiyo imewekwa mitambo maalum ya kusafisha mafuta mazito ya kulainishia injini na kuyafanya kutumika tena halikadhalika mitambo kama hiyo imewekwa pia kwa ajili ya kusafisha maji yaliyotumika kuyafanya kutumika tena.

Inafaa kuwapongeza sana wataalamu wetu kwa kuzingatia suala la usalama wa abiria na wafanyakazi wa meli hiyo kwa kuweka vifaa vya kisasa vya kujiokolea endapo kutatokea dharura pamoja na kuwekwa kwa mfumo wa usalama kwa kutumia kamera za CCTV zinazouwezo wa kuonesha takribani sehemu zote za meli zitakazosaidia kuchunga usalama wa abiria na mali zao pamoja na kuangalia uharibifu



Sehemu ya watu mashuhuri (VIP)

unaoweza kufanywa na baadhi ya watu wakiwa safarini. Aidha, jambo jengine la kufurahisha zaidi katika suala zima la usalama wa meli hiyo ni kuwekwa sehemu maalumu itayotumika kutua kwa ndege aina ya herikopta endapo kutajitokeza haja ya kufanya hivyo.

MV Mapinduzi II ni matokeo ya utekelezji wa mpango wa serikali kuimarisha usafiri wa baharini ambao umeelezwa vyema kwenye Dira ya Maendeleo 2020, MKUZA II na Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015 katika suala zima la kuimarisha miundombinu ya kiuchumi kwa lengo la kuharakisha ukuaji wa uchumi na biashara nchini.

Hata hivyo, utekelezaji wa mpango huu ulipata kasi zaidi kufuatia mfululizo wa ajali za vyombo vya bahari zilizoikumba Zanzibar kati ya mwaka 2011 na 2012, ambazo zilisababisha maafa na taharuki kubwa kutokana na maelfu ya wananchi kupoteza maisha na mali nyingi kupotea.

Mkataba wa ujenzi wa meli hiyo ulitiwa saini mwezi Julai mwaka 2013 ambapo ujenzi wake ulianza mwezi huo huo mwaka 2013 kwa kazi ya ukataji wa vyuma na usarifu wake kulikochukua miezi 12 huko katika mji wa Ulsan Kusini Mashariki mwa Korea.

Baada ya kukamilika hatua hiyo sehemu hizo zilisafirishwa hadi bandari ya Busan Kusini Magharibi ya Korea ambako ujenzi uliendelea hadi ulipokamilika mwezi Agosti, 2015.

Ununuzi wa meli hiyo unatokana na ukweli kuwa pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa na sekta binafsi katika usafiri wa baharini, bado tatizo la usafiri wa mizigo na abiria kati ya visiwa vya Unguja na Pemba na Tanzania Bara linaendelea kuwepo hasa baada ya meli mbili za Serikali MV Maendeleo na MV Mapinduzi kuchakaa na hatimae Serikali kuamua kuiuza Meli ya MV Mapinduzi.

Meli hii mpya imejengwa na Kampuni ya Daewoo International kwa kushirikiana na Kampuni ya POSCO Plantec. Ujenzi huo ulisimamiwa na Kampuni ya STX Marine ya nchini Korea ambayo iliajiriwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha ujenzi wake unafanyika kwa mujibu wa mkataba.

Ni vyema kuwaeleza wasomaji kuwa Kampuni ya Daewoo International ni miongoni mwa makampuni makubwa na mahiri ya ujenzi wa meli ambapo taarifa zinaeleza kuwa kampuni hiyo mapema mwaka 2015 ilikamilisha ujenzi wa meli kubwa kabisa duniani ya kubeba makontena.

Meli hiyo iliyopewa jina la Oscar na kumilikiwa na kampuni ya meli ya Mediterrenean ilianza safari yake ya kwanza tarehe 25 Januari, 2015. Meli hiyo ina uwezo wa kubeba makontena 19,224 yenye ukubwa wa futi 20 na kuipiku meli ya Globe ambayo imejengwa na kampuni nyingine ya Kikorea ya Hyundai. Meli hiyo inayomilikiwa na Kampuni ya China Shipping Container Lines ya Shanghai ina uwezo wa kubeba makontena 19,100 yenye ukubwa huo huo.

Kwa hivyo Serikali ilifanya uamuzi sahihi bila ya hata shaka wa kuipa kandarasi Kampuni ya Daewoo International kujenga meli hii mpya ya kisasa ya abiria na mizigo ambapo tumeelezwa kuwa ina uwezo wa kuchukua abiria 1,200 na tani 200 za mizigo ikiwemo magari 80 madogo au 50 makubwa.

Kuwasili kwa meli hii ambayo ilikuwa ikisubiriwa kwa hamu sio tu kwa wananchi wa Unguja na



Sehemu ya daraja la pili
(Business Class)



Sehemu ya daraja la tatu
(Economy Class)

Pemba bali Tanzania Bara na nchi jirani ikiwemo visiwa vya Comoro kumeleta matumaini mapya kwa wasafiri na wasafirishaji.

Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein nchini Comoro mwaka 2014, moja ya masuala yaliyojitokeza wakati wa mazungumzo yake na Rais wa nchi hiyo Dk. Ikililu Dhoinine lilikuwa usafiri wa meli kati ya Zanzibar na Comoro. Aidha, katika mazungumzo na watanzania nchini humo suala hilo lilijitokeza pia.

Kwa hivyo kukamilika kwa meli hiyo ni habari njema si kwa wananchi wa Unguja, Pemba na Tanzania Bara pekee, bali pia wananchi wa maeneo yote ya Afrika Mashariki, ambako meli hiyo itasafiri.

Safari za meli hiyo katika bandari za nchi hizo sio tu zitakuza shughuli za usafirishaji wa abiria, lakini vile vile zitakuza shughuli za biashara katika ukanda wote wa pwani ya Afrika Mashariki.

Hatuna budi kuipongeza Serikali ya Awamu ya Saba kwa kutekeleza ahadi yake ya kuimarisha usafiri wa baharini na kuonesha kwa vitendo dhamira hiyo kwa wananchi wake.

Wananchi na wadau katika sekta usafiri wa baharini wamevutiwa sana na kupata matumaini zaidi pale waliposikia kauli ya Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa meli hiyo kuwa serikali ina mpango, katika awamu hii, kununua meli nyingine mbili kwa ajili ya abiria na mizigo na nyingine ya mafuta.

Hatua hii ni ya kupongezwa sana kwa kuzingatia kuwa pamoja na kuwa lengo ni kuwapatia wananchi usafiri wa uhakika lakini pia ni sehemu ya hatua za kulifanyia mageuzi makubwa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar ili liweze kujiendesha kibiashara kama yanavyofanya mashirika mengine ya serikali kwa mfano Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Huu ni uamuzi sahihi na umekuja muda muafaka ikizingatiwa hatua nyingine ya serikali ya kujenga bandari mpya ya Mpigaduri ambayo ujenzi wake unatarajiwa kuanza mapema mwaka 2016.

Wakati wananchi na wadau mbalimbali wakiwemo wafanyabiashara wakisubiri ujenzi wa bandari hiyo ambayo itakuwa ya kisasa na kuweza kuhudumia meli nyingi na kubwa, kuwepo na shirika la Meli na Uwakala madhubuti yenye uwezo wa kutoa huduma katika bandari za mwambao wa Afrika Mashariki ni jambo lenye umuhimu wa kipekee.

Kwa hivyo ni matarajio ya wananchi na wadau mbalimbali kuwa hatua za kulifanyia mageuzi Shirika la Meli zitakwenda sambamba na mtazamo huo wa kutoa huduma zaidi kwa matazamio ya shughuli za bandari yetu mpya ya Mpigaduri.

Tunakubaliana na kauli ya Mheshimiwa Rais kuwa ufanisi wa utekelezaji wa mipango hii ya Serikali ya kuimarisha usafiri wa baharini unategemea sana na mwamko na wananchi kuwa tayari na kujidhatiti kushirikiana na serikali katika kufikia lengo hili.

Miongoni mwa wajibu wa wananchi katika hili ni kuhakikisha kuwa wanakuwa watumiaji wazuri wa meli hizo kwa kuwa watu wanaojali meli na mali za serikali kwa kuzitunza. Ni vyema wananchi wakafahamu kuwa fedha zilizotumika kununulia meli hiyo ni jasho lao hivyo ni vyema wakaitunza ili iweze kutumika kwa muda mrefu.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Nahodha wa Meli mpya ya MV - Mapinduzi II Abubakar Mzee wakati walipofika katika sehemu maalumu ya kutulia Herikopta, maelezo hayo yalitolewa katika shamra shamra za sherehe za uzinduzi wa Meli hiyo tarehe 12 Disemba 2015, katika Bandari ya Malindi Mjini Zanzibar

Ni matumaini yetu vile vile kuwa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar litafanya jitihada za kuwaelimisha wananchi sio tu wakati wakiwa safarini lakini pia kupitia vyombo vya habari juu ya namna bora ya kutunza meli hiyo ikiwemo matumizi ya vifaa mbalimbali kama vile vyoo, mifereji pamoja na viti.

# Kijini, Mbuyu Tende wapata umeme

Usambazaji wa umeme vijijini ni moja kati ya mafanikio makubwa ya uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Awamu ya Saba. Tarehe 20 Oktoba, 2015 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alizindua mradi wa umeme wa katika vijiji vya Kijini na Mbuyu Tende katika Mkoa wa Kaskazini Unguja. Katika Makala hii Jarida la Ikulu linaelezea zaidi.

Ilikuwa ziara ya nne kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kutembelea vijiji hivyo kwa shughuli mbali mbali za maendeleo na za kijamii tangu alipofanya ziara wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka 2010.

Kama kawaida ya wananchi wa kijiji cha Kijini, Rais wa Zanzibar alipokelewa na wananchi kijiji hicho wakionyesha nyuso za matumaini makubwa kunakoashiria kumuunga mkono kiongozi wao na Serikali yao. Ujio wake mara hii ni maalum kuzindua mradi wa umeme ambao ni moja ya ahadi za Serikali kwa wananchi wa vijiji hivyo.

Ni tukio la kihistoria kwa wananchi wa vijiji vya Kijini na Mbuyu Tende kwani kwa kuwepo kwa huduma hiyo kutafungua ukurasa mpya wa maendeleo katika vijiji hivyo na vijiji jirani ambavyo huduma hiyo itazidi kusambazwa.

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais katika hotuba yake fupi kwa wananchi na viongozi waliohudhuria hafla hiyo kuwa mbali ya kusaidia kuimarisha maisha ya wananchi hao lakini pia kuwepo kwa huduma hiyo kutarahisisha utekelezaji wa mipango mingine ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa katika eneo hilo.

Mfano wa mipango hiyo ni mradi mkubwa wa kitalii utakaogharimu dola za kimarekani milioni 220 ambao utajumuisha ujenzi wa nyumba za kisasa, mahoteli, kiwanja cha ndege pamoja na kiwanja cha mchezo wa gofu.

Kwa hivyo kuwepo kwa huduma ya umeme katika eneo hilo ni jambo la muhimu na ni nyenzo muhimu katika kuvutia shughuli nyingine za kitalii ambazo bila ya shaka zitasaidia sana kuviendeleza vijiji vyote vilivyo jirani na mradi huo.

Ni matumaini ya Serikali kuwa wananchi wataitumia vyema fursa ya kuwepo huduma hiyo katika vijiji vyao kujiendeleza kiuchumi kwa mfano kutumia mashine katika shughuli zao mbalimbali za kijasiriamali kuongeza uzalishaji na tija ambapo kwa upande wa shughuli zao za uvuvi kutumia



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akibonyeza kitufe ikiwa ni ishara ya Ufunguzi wa Umeme katika kijiji cha Matemwe Mbuyutende na Kijini, Wilaya ya Kaskazini A Mkoa wa Kaskazini Unguja, tarehe 20 Oktoba 2015. Kushoto ni Meneja wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZEC) Hassan Ali Mbarouk

majokofu kuhifadhi samaki wakisubiri masoko.

Kwa upande wao, kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais, kinamama watalazimika "kuongeza kasi ya ujasiriamali kwa kubuni miradi itakayokwenda sambamba na mahitaji na mabadiliko yatakayokuja"

Uzinduzi wa mradi wa umeme katika vijiji vya Kijini na Mbuyu Tende ambao umegharimiwa na Serikali kwa jumla ya shilingi milioni 263 ni mwendelezo wa kasi kubwa ya usambazaji wa umeme vijijini na miundombinu mingine ya kiuchumi ambayo ni moja ya mafanikio makubwa ya uongozi wa Awamu ya Saba.

Wakati uzinduzi huo unafanyika tayari usambazaji umeme vijijini kwa kipindi cha miaka mitano 2010-2015 ulishapita malengo kutoka vijiji 123 hadi vijiji 129.

Sambamba na umeme vijijini lakini pia Serikali imepiga hatua kubwa katika kutekeleza ahadi yake ya kuvipatia umeme visiwa vidogo vidogo ninavyokaliwa na watu.

Taarifa zinaonesha kuwa kwa sasa kwa upande wa Pemba ni visiwa vya Fundo na Shamiani tu ndio havijafikishiwa umeme baada ya visiwa vya Kojani, Kisiwa Panza na Makoongwe kupatiwa huduma hiyo wakati kwa kisiwa cha Unguja visiwa vya Tumbatu na Uzi tayari vina huduma hiyo.

Wakati akizindua mradi huo Mheshimiwa Rais alieleza dhamira ya Serikali anayoingoza kuendelea na kasi ya usambazaji umeme hadi kila sehemu wanapoishi watu huduma hiyo iwe inapatikana.

"Tunataka kuhakikisha umeme unapatikana kila sehemu wanazoishi wananchi katika kipindi cha miaka mitano ijayo" aliwaambia wananchi.

Katika mnasaba huu tunaungana na wito wa Mheshimiwa Rais kwa wananchi hao wa kuwataka kuthamini jitihada hizi za Serikali yao katika kuwaletea maendeleo kwa kushirikiana nayo kwa kuzitumia vyema huduma hizo ikiwemo kuzitunza.

Tunapenda kuipongeza Serikali kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kwa kuweka mpango madhubuti wa kuwakopesha wananchi gharama za kuunganisha umeme hatua ambayo sio tu inawahamasisha wananchi kujipatia huduma hiyo lakini pia inadhihirisha dhamira ya kweli ya Serikali ya kuwapatia wananchi wake huduma hiyo.

Kwa hivyo ni jukumu la ZECO kutekeleza mara moja agizo la Mheshimiwa Rais la kuwataka kufanya jitihada za kutoa elimu kwa wananchi juu ya namna ya kuweza kufaidika na huduma hizo ili wananchi wengi waweze kuitumia fursa hiyo na hatimaye kuondokana na umasikini.

Kwa kufanya hivyo hatua hiyo itakuwa ya msaada mkubwa kwa wananchi kwa kuwa wengi zaidi wataweza kupata huduma hiyo hivyo kuharakisha utekelezaji wa lengo la Serikali la kuwapatia wananchi wote huduma ya umeme kila mahala walipo.

Kwenu wananchi wa Kijini na Mbuyu Tende wakati ndio huu "shime changamkieni fursa hizo"kama alivyowataka Mheshimiwa Rais katika hotuba yake wakati anazindua mradi wa umeme.

# Zanzibar yapata Tunzo ya dhahabu




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiiangalia Tunzo ya dhahabu iliyopewa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ( Gold Future Policy Award kwa mwaka 2015) ambayo imetolewa na Taasisi ya kimataifa ya World Future Council katika Mji wa Geneva Uswizi tarehe 20 Oktoba, 2015 baada ya Sheria ya Watoto ya Zanzibar ya Mwaka 2011 kuzishinda sheria za Nchi nyingine zaidi ya 20 kwa kukidhi vigezo vilivyoshindaniwa. Hafla ya makabidhiano hayo ilifanyika tarehe 26 Novemba, 2015, Ikulu Mjini Unguja,

Tarehe 26 Novemba, 2015 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alikabidhiwa rasmi tuzo ya dhahabu iliyopewa Sheria ya Watoto ya Zanzibar ya Mwaka 2011 na taasisi ya kimataifa ya World Future Council.

Tunzo hii ni matokeo ya kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na washirika wake wa ndani na nje katika kuimarisha haki na ustawi wa watoto nchini kupitia sera, sheria na mikakati ya utekelezaji wake.

Taasisi ya Kimataifa ya World Future Council inajishughulisha na kushajiisha uandaaji na utekelezaji wa sera zinazolenga kuimarisha ustawi, haki na hali za maisha kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Kwa hivyo ili kuhamasisha kufikia malengo hayo, kwa miaka

mingi sasa, taasisi hiyo imekuwa ikitoa tunzo kwa nchi na taasisi ambazo zimekuwa zikitunga na kutekeleza vyema sera, sheria na mipango ambayo inakwenda sambamba na azma yake ya kuleta na kuimarisha maendeleo endelevu na mustakabala wa jamii.

Kwa mwaka 2015, taasisi hii ilielekeza jicho lake katika sera na sheria zenye kuchangia ulinzi na kuimarisha haki za watoto wote wa kike na wa kiume, ambapo jumla ya sera na sheria za nchi 20 zilishindanishwa.

Zanzibar ilikabidhiwa tunzo hiyo katika sherehe zilizofanyika mjini Geneva, Uswizi tarehe 20 Oktoba, 2015 ambapo Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto Bi Asha Ali Abdalla aliongoza ujumbe wa Zanzibar.

"Tumeshinda tunzo hii kwa kuwa Sheria ya Watoto Zanzibar imekidhi vigezo vinavyokubalika kimataifa pamoja na namna mchakato wetu wa kutengeneza sheria hii hadi kupitishwa kwake kuwa shirikishi" alibainisha Bi. Asha Ali Abdalla, Katibu Mkuu Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Sheria hii ya watoto Zanzibar imezingatia viwango/vigezo vinavyotambuliwa na Sheria ya Watoto ya Umoja wa Mataifa ya Mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Watoto wa Mwaka 1990. Chini ya sheria hii watoto ama wakiwa watuhumiwa wa makosa au mashahidi wanapewa ulinzi wa kisheria na haki nyingine zikizingatiwa ikiwemo matunzo yao na ulinzi kizuizini.

Bila ya shaka pamoja na ubora wa sheria hiyo na mchakato shirikishi uliofanikisha utungwaji wake, lakini hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutekeleza sheria hiyo tangu ilipopitishwa mwaka 2011 zimechangia sana kupata ushindi huo.

Ni dhahiri tangu uongozi wa Serikali ya Awamu ya Saba kuingia madarakani mwaka 2010 kumekuwepo na jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa haki za watoto zinaheshimiwa na ustawi wao unalindwa.

Jitihada hizo zinatokana na ukweli kuwa kumekuwepo na vitendo vingi vya uvunjaji wa haki za watoto na wanawake katika jamii yetu ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia hivyo kupitishwa kwa sheria hiyo ilikuwa moja ya hatua muhimu za kukabiliana na vitendo hivyo.

Mara baada ya kupitishwa sheria hiyo hatua nyingine zilifuata ambazo ni pamoja na uanzishwaji wa mahkama za watoto, vituo vya mkono kwa mkono katika baadhi ya hospitali vinavyosaidia wahanga wa vitendo vya udhalilishaji watoto na kuanzisha madawati ya jinsia katika vituo vya Polisi kushughulikia masuala ya udhalilishaji wa watoto na wanawake.

Katika jitihada hizo za Serikali, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amekuwa na mchango mkubwa ambapo katika kipindi chake cha uongozi alizindua rasmi kampeni kubwa dhidi ya unyanyasaji na udhalilishaji watoto nchini.

Kampeni hii ambayo imekuwa ikiendelezwa na Mheshimiwa Rais kila mara katika hotuba zake sehemu mbalimbali imechangia sana kupata mafanikio kwa Sheria ya Watoto Zanzibar.

Mwaka 2013 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na washirika mbalimbali wa ndani na nje imeweza kukamilisha Mkakati wa Miaka Mitano wa Mapitio na Marekebisho ya Sheria ya Watoto (Child Justice Reform: A five year Strategy 2013-2018).

"Tunzo hii imesaidia sio tu kuitangaza Zanzibar bali pia imedhihirisha utashi na dhamira ya kisiasa ya viongozi wa Zanzibar katika kusimamia sheria na kupanga mikakati inayolenga kuhakikisha haki na ustawi watoto nchini" Bi Asha Abdalla alisema katika maelezo kwenye hafla ya kukabidhi tunzo hiyo.

Katika shindano la mwaka 2015 mbali ya Zanzibar kunyakua tunzo ya dhahabu, tunzo nyingine mbili za fedha zilitolewa kwa nchi zilizofanya vizuri.

Finland kupita sheria yake ya Elimu ya Msingi (Basic Education Act) ya mwaka 1998 ilijinyakuliwa tunzo ya fedha. Sheria hiyo, kwa mujibu wa Taasisi ya World Future Council, inawahakikishia watoto fursa sawa ya elimu bora na mafunzo bila kujali uwezo (utajiri), rangi, umri, lugha au mtu alipo. Matokeo ya sheria hiyo ni nchi ya Finland kupata alama za juu katika majaribio ya kimataifa.

Jimbo la Meryland nchini Marekani lilijinyakulia pia tunzo ya fedha kutokana na mafanikio kwa kuweka kigezo cha ufahamu wa elimu ya mazingira kuwa sharti la kwa watoto wanaomaliza elimu ya sekondari (Environmetal Literacy Standards).

Kwa hakika tunzo hii kwa Zanzibar ni kielelezo cha matokeo ya kazi nzuri iliyofanywa kwa ushirikiano mkubwa kati ya watu na taasisi mbalimbali nchini na nje kwa maslahi mapana ya Zanzibar na watu wake.



# Ujenzi wa Mji Mpya Fumba umeanza

Njia mpya inayoelekea katika Mji Mpya wa Fumba itakayokuwa na upana wa mita 50 ambao utaruhusu kupishana kwa gari kumi kwa wakati mmoja

Zaidi ya miaka 20 baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutangaza azma yake ya kuyaendeleza maeneo huru ya kiuchumi, utekelezaji wa mpango huo sasa umeonesha mwelekeo baada ya shughuli mbali mbali kuanza kufanyika kwenye maeneo hayo.

Hatua hiyo ni sehemu ya mafanikio ya juhudi za serikali zinazolenga kuifanya Zanzibar kuwa ya kisasa zaidi yenye kufikia kiwango cha uchumi wa kipato cha kati kwa wananchi wake kwa kujenga mazingira bora ya uwekezaji wenye manufaa zaidi kiuchumi na kijamii nchini.

Dhamira ya Serikali katika kujenga mazingira yatakayoiwezesha Zanzibar kupiga hatua zaidi za kimaendeleo kwa kushirikiana na sekta binafsi ilianza tokea mwaka 1994, ilipotangaza rasmi kutenga maeneo matano. Maeneo hayo ni eneo la Fumba, Micheweni ambalo linajumuisha Kiuyu na Maziwa Ng'ombe, Eneo la Viwanda la Amani, Uwanja wa Ndege na Maruhubi.

Lakini pamoja na nia nzuri iliyokuwepo ya kuyashughulikia maeneo hayo, utekelezaji wa mpango huo tokea ilipotangazwa nia hiyo umekuwa ukishindikana kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo Serikali kushindwa kupata fedha za kuyaendeleza maeneo hayo.

Moja kati ya maeneo yaliyopata msukumo mkubwa katika siku za hivi karibuni kuyaendeleza maeneo hayo ni ujenzi wa miundombinu katika eneo la Fumba.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein kwa kushirikiana na muwekezaji mzalendo Bwana Said Salim Bakhresa kwa pamoja wanaliendeleza eneo la Fumba kwa kuanza kujenga kiwanda cha kisasa cha maziwa pamoja na miundombinu itakayoshajiisha wawekezaji kuwekeza kwenye eneo hilo.

Eneo la Fumba ambalo limetengwa kwa madhumuni hayo ya uwekezaji lina ukubwa wa hekta 3000. Kwa mujibu wa mpango wa matumizi ya ardhi, eneo hilo la Fumba limegawiwa makundi matatu makubwa; eneo la vijiji vya asili hekta 800,

eneo la majengo ambalo nalo limegaiwa katika maeneo matatu tofauti. Eneo moja ni eneo la uendelezaji miradi ya kibiashara - "Fumba Town Development" – Nyamanzi hekta 60, Eneo la pili ni mradi wa ujenzi wa nyumba za kati - Fumba Kororo hekta 76 na eneo la tatu ni ujenzi wa mji mpya wa kisasa wa kibiashara hekta 700.

Ili kuhamasisha utekelezaji wa mradi huo, tarehe 22 Novemba 2015, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alitembelea eneo hilo kukagua shughuli mbali mbali za miradi ya uwekezaji inayoendeshwa na makampuni ya Bakharesa.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kwa ufupi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Uekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) Ndugu Salum Khamis Nassor wakati alipotembelea maeneo ya ujenzi wa mji mpya wa nyumba za kisasa zinazojengwa na Kampuni ya "Azam Group of Companies" katika kijiji cha Fumba Wilaya ya Magharibi B Unguja, tarehe 22 Novemba, 2015

"haya ndio maendeleo tunayoyataka na hatuna budi kuyatangaza ili watu walijue eneo hili la Fumba lenye mwelekeo mpya kabisa wa maendeleo ya kisasa" alisema Dk. Shein.

Mara baada ya kufika kwenye eneo hilo, Rais wa Zanzibar alipatiwa maelezo kuhusiana na mradi huo. Jambo la kwanza kubwa linaloweza kuonekana mara tu baada ya kuingia kwenye eneo hilo, ni bara bara yenye upana wa mita 50, ambayo ipo kwenye kiwango cha lami ya awali.

Pembezoni mwa bara bara hiyo kuna ujenzi unaoendelea wa kituo cha habari na mawasiliano ambacho kitatumika kutoa taarifa mbali mbali za ndani na nje ya nchi kuhusiana na masoko na matukio tofauti.

Kiwanda kikubwa cha kisasa cha maziwa kimejengwa pembezoni mwa eneo la mradi wa ujenzi wa nyumba ambapo miundo mbinu ya barabara inaenelea kujengwa.

Ziara ya Rais wa Zanzibar ilimpeleka hadi kwenye ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kokoto chenye uwezo wa kuzalisha tani 120 za kokoto kwa saa. Pembezoni mwa kiwanda hicho kulikuwa na ujenzi unaoendelea wa kiwanda kipya cha kutengenezea lami.

Kwa mujibu wa Bwana Said Salim Bakhresa, viwanda hivyo vitazalisha lami na kokoto ambayo itatosheleza kwa mahitaji ya kampuni yake na makampuni mengine yatakayoendeleza ujenzi kwenye eneo hilo. Vile vile alitembelea sehemu itakayojengwa nyumba 500 za aina na ukubwa tofauti pamoja na huduma nyingine za kijamii, ujenzi wa gati ndogo na mitambo ya ujenzi wa barabara.

Dk. Shein aliupongeza uongozi wa Makampuni ya Bakhresa chini ya kiongozi wake Sheikh Said Bakhresa kwa kuonesha mfano katika uwekezaji katika mradi huo mkubwa ambao sio tu utaibadilisha kabisa haiba ya mji wa Fumba lakini pia utaipatia sifa zaidi Zanzibar.

Katika maelezo yake kwa Mheshimiwa Rais, Mwenyekiti wa Makampuni ya Bakhresa Sheikh Said Salum Bakhresa alieleza kuwa awamu ya kwanza ya mradi huo utakaogharimu zaidi ya dola za kimarekani milioni 100, utahusisha ujenzi wa nyumba 100.

Aidha, alipata maelezo kuhusiana na ujenzi wa gati ndogo ambayo itawezesha vifaa na mahitaji mengine ya mradi kwenda Fumba moja kwa moja. Baada ya mradi huo kukamilika, bandari hiyo itaimarishwa ili itumike kwa shughuli za kusafirishia abiria na mizigo.

Ziara ya Dk. Shein ilikamilika baada ya kuangalia ramani za majengo na maeneo yote ya eneo hilo ikiwemo viwanja vya michezo na burudani na kupatiwa maelezo ya kina kuhusiana na mradi huo na namna ambavyo wawekezaji wanaweza kuvutiwa kuwekeza biashara zao.




Rais wa Zanzinbar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kwa ufupi kutoka kwa Mwenyekiti wa Kampuni ya Azam Bw. Said Salim Bakhresa alipowasili katika eneo linalotarajiwa kujengwa kiwanda cha utengezaji wa Lami katika Kijiji cha Fumba Mkoa wa Mjini Magharibi katika ziara ya kutembelea maeneo ya ujenzi wa Mji mpya wa Nyumba za kisasa zinazojengwa na Kampuni ya Azam Group kwa kushirikiana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, tarehe 22 Novemba, 2015



Rais wa Zanzinbar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kwa ufupi kutoka kwa Mwenyekiti wa Kampuni ya Azam Bw. Said Salim Bakhresa alipowasili katika eneo linalotarajiwa kujengwa kiwanda cha utengezaji wa Lami katika Kijiji cha Fumba Mkoa wa Mjini Magharibi katika ziara ya kutembelea maeneo ya ujenzi wa Mji mpya wa Nyumba za kisasa zinazojengwa na Kampuni ya Azam Group kwa kushirikiana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, tarehe 22 Novemba, 2015

# Ziara ya Dk. Shein ya India imezaa Matunda

■ Chuo cha taaluma ya mafunzo ya amali kimezinduliwa Kibokwa



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia kazi za utengenezaji vifaa vya umeme wa jua zinazofanywa na wanafunzi wa kituo cha kuwafunza Wanawake wakati wa sherehe za ufunguzi wa kituo hicho katika kijiji cha Kibokwa Wilaya ya Kaskazini A, tarehe 6 Agosti, 2015

Tarehe 6 Agosti, 2015 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alizindua rasmi kituo cha kutoa mafunzo ya elimu ya amali na ujasiriamali kwa kinamama huko Kibokwa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Jarida la Ikulu linaeleza umuhimu wa kituo hicho katika kuchochea maendeleo ya kinamama na jamii kwa ujumla.

Ilikuwa ni siku ya furaha kubwa kwa wakaazi wa kijiji cha Kibokwa kilichopo kiasi ya kilomita 35 kutoka mjini Unguja ambapo kijiji hicho kilipata ugeni mzito wa watu kutoka pande mbalimbali za nchi yetu na nje. Ugeni huo pamoja na wenyeji walipamba sherehe kubwa ya uzinduzi wa Kituo cha Mafunzo ya Elimu ya Amali na Ujasiriamali kwa Kinamama.

Kituo hiki ni matokeo ya ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Rais aliyoifanya nchini India mwezi Februari, 2014. Akiwa nchini humo alipata fursa ya kutembelea chuo kama hicho kinachoitwa Barefoot kilichoko katika kijiji cha Tilonia, wilaya ya Ajmer, jimbo la Rajastan. Kituo hicho kinafundisha kinamama kazi za amali na ujasiriamali.

Mheshimiwa Rais alivutiwa sana na mchango wa chuo hicho katika kuwawezesha kinamama kujiletea maendeleo kwa kuwapatia ujuzi na nyenzo za kukabiliana na changamoto za maisha yao ya kila siku ikiwemo kupambana na umasikini.

Katika mnasaba huo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Uongozi wa chuo hicho ulitia saini makubaliano ya kuanzisha chuo kama hicho Zanzibar hivyo uzinduzi wa kituo hicho ni matokeo ya makubaliano hayo.

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya uzinduzi, kituo hicho ni moja ya hatua muhimu za utekelezaji wa mipango ya serikali ya kuimarisha maendeleo ya wanawake, ujasiriamali na kutengeneza



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifuatilia kwa makini maelezo yanayotolewa na mmoja kati ya wanafunzi wa kituo cha kuwafunza Wanawake utengenezaji wa vifaa vya Umeme wa jua na kazi mbali mbali za ujasiriamali katika kijiji cha Kibokwa Wilaya ya Kaskazini A, tarehe 6 Agosti, 2015

ajira ili kuwawezesha wanawake kupambana na umasikini.

Kwa hakika kuna kila sababu za kuzipongeza jitihada za Serikali ya Awamu ya Saba chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dk. Shein kwa namna ambavyo imekuwa ikifanya jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa wanawake nchini wanapata fursa za kujiendeleza kadri inavyowezekana kulingana na nafasi na mchango wao katika jamii.

Jitihada hizi za serikali ni sehemu ya utekelezaji wa malengo mbalimbali ya uimarishaji wa hali ya maisha ya kinamama kama yalivyoainishwa katika mipango ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Dira ya Maendeleo Zanzibar 2020, MKUZA II, Ilani ya Uchaguzi wa CCM 2010-2015 pamoja na Malengo ya Milenia.

Hivyo ni vyema kauli ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraz la Mapinduzi kuwa Wazanzibari wana kila sababu za kujivunia hatua kubwa ya maendeleo iliyofikiwa katika kuimarisha hali ya kinamama katika kipindi hiki cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Saba ikaungwa mkono kwa juhudi zote ili kuleta mafanikio zaidi.

Kwa hivyo kuzinduliwa kwa chuo hiki ni hatua nyingine muhimu katika kuongeza kasi ya maendeleo ya kinamama nchini pamoja na jamii kwa ujumla kwa kuwa lengo la mafunzo yatakayotolewa kituoni hapo ni kuwa chachu ya maendeleo ya nchi yetu kwa kuamini fika usemi wa wahenga 'ukimuelimisha mwanamke mmoja, basi umeelimisha jamii' hivyo ukimuimarisha/ukimwezesha mwananke umeimairisha/ umeiwezesha jamii.

Kama hivi leo Zanzibar inajivunia mafanikio makubwa ya watoto wa kike katika elimu ya sekondari na vyuo vikuu, basi katika miaka michache ijayo tunatarajia matokeo mazuri zaidi kwa kuwa mchango wa kituo hiki kuimarisha hali za kinamama utatoa fursa zaidi kwa watoto wa kike na kiume kupata huduma / mahitaji yao zaidi ya kielimu na mengine kutoka kwa wazazi wao watakaowezeshwa kupitia kituo hiki.

Kukamilika kwa kituo hiki kutatoa fursa zaidi kwa kinamama nchini kujiendeleza katika fani mbali mbali za ujasiriamali ikiwemo ufundi wa vifaa vya umeme wa jua na usambazaji wake, ushoni, ufugaji wa nyuki kwa ajili ya asali, ukulima wa mboga mboga na utengenezaji wa bidhaa kama vile chaki na vyandarua.

Kama alivyobainisha Mwakilishi wa Shirika la Umoja



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikabidhiwa kitenge maalum na aliekuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto Bwana Ali Khamis Juma wakati wa sherehe za ufunguzi wa kituo cha kuwafunza Wanawake utengenezaji wa vifaa vya Umeme wa jua na kazi mbali mbali za ujasiriamali katika kijiji cha Kibokwa Wilaya ya Kaskazini A, tarehe 6 Agosti, 2015

wa Mataifa linaloshughulikia wanawake (UN Women) nchini Bibi Anna Collins, katika pongezi zake kwa Serikali, kuwa kituo hiki ni mfano bora wa uwezeshaji kinamama kiuchumi katika mtazamo mpana wa maendeleo endelevu ambao unajielekeza katika kuleta usawa wa jinsia, kuondoa umasikini na ukuaji wa uchumi unaoshirikisha/ unaomgusa kila mwananchi.

Bibi Collins alibanisha kuwa kituo hiki kinaongeza sauti ya kinamama kusikika na uhuru wao katika jamii kitu ambacho kinajenga matumaini ya kutimiza ndoto zao za maisha hivyo kuongeza hamasa kwa vijana kujiamini na kujituma zaidi.

Jambo jingine muhimu ni kuwa mafunzo wanayoyapata kinamama katika kituo hicho yanawapa kinamama uwezo wa kujiamini na kuwawezesha kupanga, kutekeleza na kufanya maamuzi sahihi katika kutekeleza shughui zao mbalimbali za kujipatia kipato pamoja na maendeleo ya jamii katika maeneo yao.

Ni vyema kueleza kuwa kituo hiki ni cha aina ya kipekee kwa kuwa kinamama wanaojiunga na kituo hiki ni wale wa maeneo ya vijijni ambao ama hawakupata fursa ya elimu au wamefikia kiwango kidogo cha elimu. Watu hao mara nyingi katika jamii zetu huonekana kuwa ni watu wasioweza kufundishika tena jambo ambalo husababisha baadhi yao kukata tamaa katika maisha.

Kituo hiki kimejengwa kwa ushirikiano kati ya serikali na washirika wa maendeleo ambapo jumla ya shilingi milioni 124.5 zilitumika kukarabati majengo ambapo kati ya hizo milioni 76.3 zilitolewa na serikali na shilingi milioni 48.2 zimetolewa na UN-Women.

Mshirika mkuu Chuo cha Barefoot India kimegharimia ununuzi wa samani, uchimbaji wa kisima, ujenzi wa tangi la kuvuna maji ya mvua lenye uwezo wa kuhifadhi lita 30,000 pamoja na matangi ya maji ya moto yanayotumia umeme jua. Aidha, Taasisi ya Milele Zanzibar ni miongoni mwa taasisi zilizoshiriki katika uanzishwaji wa kituo hiki.

Malengo ya muda mrefu ni kituo hiki kupokea kinamama kutoka nchi jirani. Hiyo ni fursa nyingine kwa wananchi wa Zanzibar kuonesha utamaduni wetu ulioambatana na ukarimu ili kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati yetu na majirani zetu.

# Matukio katika Picha



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Balozi mteule nchini Zimbabwe Luteni Jenerali Mstaafu Charles Makakala Ikulu Zanzibar tarehe 21 Agosti, 2015



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na Mkurugenzi wa Shirika la Misada la Uengereza (DFID) Vel Gnanendran alipofika Ikulu Mjini Zanziba tarehe 24 Oktoba, 2015. Aliesimama katikati ni Balozi wa Uengereza nchini Tanzania Bi Dianna Melrose



Rais wa Zanzibar wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifungua pazia katika jiwe la msingi ikiwa ni ishara ya kulifungua Jengo jipya la Wizara ya Katiba na Sheria liliopo Mazizini Nje kidogo ya Mji wa Zanzibar, tarehe 06 Oktoba 2015. Kushoto ni Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakari na (kulia) Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndugu Asaa Omar Hamad



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akizungumza na Balozi wa Msumbiji nchini Tanzania Vicente Mebunia Veloso Ikulu Mjini Zanzibar tarehe 3 Agosti, 2015



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimsikiliza Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati Mh. Ramadhan Abdallah Shaaban akitoa maelekezo kuhusu mradi wa maji safi na salama wakati alipotembelea mradi wa uimarishaji maji safi na salama kwa uchimbaji wa kisima kipya na ukarabati wa tangi la maji Makunduchi Wilaya ya Kusini Mkoa wa Kusini Unguja, tarehe 01 Disemba, 2015



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na mkewe mama Mwanamwema Shein wakiangalia machapisho mbali mbali yanayotoa elimu kwa wananchi kuhusu bidhaa zinazotokana na karafuu katika banda la maonesho ya bidhaa za karafuu. Maonesho hayo yalifanyika katika kiwanda cha Makonyo Wawi Wilaya ya Chechake Pemba tarehe 26 Ogasti, 2015

# Uzinduzi wa miradi ya Maendeleo Pemba

Mwishoni mwa mwezi wa Agosti Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alifanya ziara ya siku nne kisiwani Pemba. Ziara hiyo ambayo ilikuwa mahsusi ilikamilika baada ya kuzindua miradi kadhaa pamoja na kuweka mawe ya msingi ya miradi mipya. Katika makala hii gazeti lako linakupitisha katika ziara hiyo hatua kwa hatua.

Miradi iliyokuwemo katika ziara hiyo ni ya sekta ya elimu, maji, afya, miundombinu, kilimo, maliasili na mazingira, michezo na burudani.

Ni hatua nzuri ya mafanikio katika sekta hizo kisiwani Pemba ikiwa ni matokeo ya utekelezaji wa malengo yaliyomo katika mipango ya maendeleo ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar Awamu ya Pili (MKUZA II), Malengo ya Milenia na Ilani ya Uchaguzi ya CCM mwaka 2010-2015.

Katika maelezo yake kwa wananchi, Dk. Shein alisema mafanikio yaliyopatikana Unguja na Pemba katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake ni matokeo ya amani na utulivu uliopo pamoja na ushirikiano kati ya serikali na wananchi, hivyo aliwasihi wananchi kuendelea kudumisha hali hiyo kwa kuzidisha upendo miongoni mwao.

## Uzinduzi wa Tawi la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kimepiga hatua nyingine mbele katika kujiimarisha baada ya kukamilisha ujenzi wa Tawi la chuo hicho, Kampasi ya Benjamin Mkapa, huko katika kijiji cha Mchangamdogo Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini, Pemba.

Sherehe za uzinduzi wa Tawi hilo ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein zilifana sana ambapo mamia ya wanafunzi na wananchi wa vijiji vya jirani walihudhuria.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikata utepe kuzindua Tawi la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) katika Chuo cha Benjamin Willium Mkapa liliopo Mchanga mdogo Kaskazini Pemba tarehe 25 Agosti 2015. Kulia ni Mke wa Rais Mama Mwanamwema Shein na kushoto ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mheshimiwa Ali Juma Shamuhuna

Kampasi hiyo kwa mujibu wa Makamu Mkuu wa Chuo hicho Profesa Idrisa Ahmada Rai, itaanza kwa kuendeleza masomo ya Ualimu katika ngazi ya Diploma ya Msingi yanayotolewa Chuoni hapo na mafunzo mengine ya muda mfupi kwa taaluma mbali mbali kama vile masomo ya matumizi ya teknolojia ya Tehama, mafunzo ya ujasiriamali na mafunzo ya lugha za kigeni.

Kama walivyosema wahenga ‘mwanzo wa hesabu ni moja’ lakini lengo la muda mrefu ni kuona mengi ya masomo yanayofundishwa katika kampasi nyingine zilizoko Unguja kuanzia shahada ya kwanza hadi shahada ya uzamivu yanatolewa pia katika kampasi hiyo.


Kwa hivyo kuzinduliwa tawi hilo lenye majengo ya kisasa na huduma zote za msingi kwa wanafunzi kisiwani Pemba ni hatua nyingine muhimu ya kuimarisha maendeleo ya elimu ya juu katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Hatua hii inakwenda sambamba na utekelezaji wa malengo ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 na sababu kuu ya kutangazwa elimu bila ya malipo mara tu baada ya Mapinduzi hayo.

Kama alivyoeleza Dk. Shein katika hotuba yake ya uzinduzi kuwa kampasi hiyo ni fursa nyingine kwa vijana wa kisiwa cha Pemba kupata elimu ya juu kisiwani humo tofauti na huko



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia moja ya darasa katika Tawi la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) katika Chuo cha Benjamin Willium Mkapa, Mchanga mdogo Kaskazini Pemba baada ya kufanya uzinduzi rasmi tarehe 25 Agosti 2015



nyuma ambako walilazimika kufuata elimu ya juu katika vyuo vilivyoko Unguja, Tanzania Bara na hata nchi za nje. Kwa hivyo Tawi hilo la SUZA litakuwa kichocheo cha kuharakisha mabadiliko katika jamii na kuleta maendeleo.

Kuongezeka kwa Kampasi ya Benjamin Mkapa kunafanya chuo hicho sasa kuwa na kampasi nne. Kampasi nyingine ni Tunguu, Vuga na Nkrumah. Ni matarajio kwa serikali kuwa kuwepo kwa kampasi hizo kutatoa changamoto kwa vijana kuzitumia vyema fursa za elimu ambapo sasa wamerahisishiwa kwa kuzidi kusogezewa huduma za elimu mahala walipo.

Ni ukweli usiopingika kuwa katika kipindi hiki cha uongozi wa awamu ya kwanza ya serikali ya Awamu ya Saba Chuo hicho chenye umri wa miaka 14 sasa kimepanuka kwa haraka sana kitaasisi na kitaaluma hivyo kuweza kwenda sambamba na mabadiliko na mahitaji ya elimu ya juu katika nchi yetu.

Kwa hivyo hatuna budi kuupongeza kwa dahati uongozi wa SUZA kwa mafanikio hayo makubwa yaliyopatikana katika kipindi hiki kifupi.

Lakini shukrani za pekee hazina budi kuelekezwa kwa Mkuu wa Chuo hicho ambaye pia ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa jitihada zake binafsi katika kuhakikisha kuwa chuo hicho kinapiga hatua haraka iwezekanavyo na hatimae kinakuwa moja ya vyuo bora na vya kutegemewa katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Ni jambo la kujivunia kuona kuwa wakati wote panapokuwepo na fursa ya kusaidia chuo hicho Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele katika 'kukipigia debe'. Kwa mfano katika mazungumzo yake na washirika wa maendeleo iwe humu nchini au katika safari zake za kikazi nje ya nchi, SUZA ni moja ya ajenda zake muhimu katika mazungumzo na wenyeji wake zikiwemo taasisi za elimu na utafiti.

Matokeo yake SUZA hivi sasa imekuwa na mahusiano na mashirikiano na vyuo vikuu vingi pamoja na taasisi za kitafiti ambapo kinapata kubadilishana uzoefu na kufanya kazi za kitafiti na taasisi hizo na hivyo kuongeza ujuzi na taaluma kwa wakufunzi na wataalamu wa chuo.

Uwezo na uzoefu katika kufanya tafiti ni moja ya vigezo vinavyovipandisha hadhi vyuo vikuu. Hii inatokana na nafasi ya vyuo vikuu katika kuleta maendeleo. Hivyo ni wajibu wa chuo kikuu chochote ulimwenguni kufanya tafiti kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbali mbali zinazoikabili jamii sambamba na kutoa ushauri. Kutokana na sababu hiyo, ndiyo maana Mheshimiwa Rais kwenye hotuba zake amekuwa akisisitiza jambo hilo.

Katika hatua nyingine tunaungana na pendekezo lililotolewa na Makamu Mkuu wa SUZA Profesa Idrissa Ahmada Rai ya kutaka Chuo hicho kikabidhiwe skuli ya sekodari ya Mchangamdogo ambayo ipo jirani ya chuo hicho.

Pendekezo hili ni muhimu kama ilivyoelezwa SUZA inayo

skuli kama hiyo katika kampasi ya Tunguu na imekuwa ni moja ya skuli zinazofanya vyema katika mitihani ya taifa hivyo kuihakikishia SUZA wanafunzi wenye uwezo zaidi kujiunga na chuo hicho hasa katika masomo ya sayansi.

Itakuwa ni jambo la busara sana ikiwa SUZA itakabidhiwa skuli hiyo kwa faida ya jamii kuanzia mwanafunzi mmoja mmoja hadi kwa taifa kwa kuwa uamuzi huo utasaidia kupunguza pengo kubwa la wanafunzi wa masomo ya sayansi katika vyuo vya elimu ya juu nchini.

Sambamba na pendekezo hilo, ni vyema mamlaka husika ikalipa kipaumbele ombi la chuo hicho la kupatiwa eneo zaidi kwa ajili ya matumizi yake hasa ikizingatiwa kuwa kwa namna yeyote ile kampasi hiyo baada ya muda itapanuka na itahitaji eneo zaidi kwa shughuli zake.

Na itakuwa ni jambo jema kama ombi hili likatekelezwa bila ya ajizi kama wahenga walivyonena 'ajizi ni nyumba ya njaa'. Ni muhimu kuzingatia kuwa ujenzi katika maeneo mengi ya nchi yetu ikiwemo Mchangamdogo hivi sasa umeshika kasi hivyo kuchelewa kutekelezwa ombi hili sasa kunaweza ama kukwamisha kabisa upanuzi wa chuo hicho siku za baadae au zoezi hilo kufanyika kwa gharama isiyotarajiwa na ikawa 'majuto ni mjukuu'

Tunalitilia mkazo sana suala hili kwa kuzingatia ukweli kuwa kwa namna ambavyo sekta ya elimu inavyoendelea kupanuka hatutarajii kuwa SUZA itaendelea kubaki katika muundo wa sasa hivyo haitakuwa jambo la kushangaza Kampasi ya Benjamin Mkapa siku moja kikawa chuo kikuu kinachojitegemea kama historia inavyoonesha kwa vyuo vikuu vya taifa kama SUZA.

## Mradi wa Maji Safi na Salama na Mazingira Zanzibar



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifungua mfereji kuruhusu maji kuingia kwenye ndoo mara baada kufungua Mradi wa Maji safi na Salama katika kijiji cha Taif Wete Pemba Mkoa wa Kaskazini akiwa katika ziara ya kuifungua miradi mbalimbali ya Maendeleo tarehe 25 Ogasti 2015. Mradi huu umefadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika ADB,

Mradi huu ni moja kati ya miradi mikubwa ya maji iliyotekelezwa katika Awamu ya Saba, lengo likiwa ni kutekeleza kwa vitendo malengo ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 ya kuwapatia wananchi maji safi na salama. Tokea Awamu ya Kwanza lengo hili limekuwa likitekelezwa hatua kwa hatua kulingana na mahitaji na uwezo wa uchumi wa nchi. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa mradi huo, serikali haitasita kukopa ikiwa



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifungua pazia kama ishara ya uzinduzi wa Mradi wa Majisafi na salama katika kijiji cha Taif Wete Kaskazini Pemba akiwa katika ziara ya kuifungua miradi mbalimbali ya Serikali kisiwani humo tarehe 25 Agosti, 2015. Mradi huu umefadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB)

uchumi utaruhusu ili kufanikisha mipango ya maendeleo kama ilivyofanya kwa mradi huu.

Mradi huu wa Maji safi na Salama, Usafi wa Mazingira Zanzibar ambao ulitekelezwa kwa pamoja kati ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-Habitat) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulihusisha maeneo makuu manne.

Maeneo hayo ni ya Kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji ili kuiwezesha kutoa huduma bora, Ujenzi wa Miundombinu ya Kusambaza Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Unguja na Pemba, Ujenzi wa Miundombinu ya Kuimarisha na Kuendeleza huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira katika Miji Mitatu ya Pemba na Kuimarisha na Kuvitunza Vianzio vya Maji Unguja na Pemba.

Gharama za mradi huu ni jumla ya shilingi bilioni 67.73 ambapo shilingi bilioni 50.85 ni mkopo kutoka benki ya AfDB na benki hiyo ilitoa fedha nyingine shilingi bilioni 6.10 zilikuwa ni msaada. UN-Habitat ilitoa msaada wa shilingi bilioni 2.50

Kwa upande wake Serikali ilitumia shilingi bilioni 8.28 kwa ajili ya kulipa fidia mali na mazao ya wananchi yaliyoathirika na ujenzi wa maradi pamoja na kupeleka umeme katika vituo vya maji.

Kisiwani Pemba mradi huu umeongeza kiwango cha uzalishaji maji kutoka lita 14,022,000 kwa siku hadi lita 35,600,000 kwa siku kwa mkoa wa Kaskazini Pemba ikiwa ni ongezeko la asilimia 154 na kwa upande wa Mkoa wa Kusini Pemba uzalishaji maji umeongezeka kutoka lita 19,034,000 hadi lita 36,500, ikiwa ni ongezeko la asilimia 92.

Kwa ujumla kukamilika kwa Ujenzi wa Miundombinu ya Kuimarisha na Kuendeleza huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira katika miji mitatu ya Pemba (Chake-Chake, Mkoani na Wete) tayari kumewezesha wananchi 70,852 kupata huduma hiyo. Kwa upande wa vijijini wananchi wapatao 54,173 wa shehia za Wambaa, Chumbageni, Mizingani, Ndagoni, Wesha, Vitongoji (ikiwemo Uwandani na Kibokoni), Ng'ambwa, Mchangamodogo, Kiswani, Piki, Mzambarauni na Chwale nao wanapata huduma hiyo

Kwa upande wa kisiwa cha Unguja, mradi umewafaidisha wananchi wapatao 41,000 kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji maji kwa asilimia 53 kutoka lita 14,952,000 hadi lita 22,900,000 kwa siku kwa mkoa wa Kaskazini wakati katika mkoa wa Kusini uzalishaji umeongezeka kwa asilimia 5 kutoka lita 13,574,000 kwa siku hadi lita 14,300,000.

Kutokana na mafanikio ya utekelezaji wa mradi huo, Mheshimiwa Rais alizipongeza jitihada za wizara ya Ardhi, Makazi, Maji na Nishati kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikiifanya ambayo imewezesha Zanzibar kuzalisha lita milioni 163 za maji ikiwa ni asilimia 76 ya mahitaji yake ambayo hadi Disemba 2014 yalikuwa ni lita 214,580,240.

Dk. Shein aliwaambia mamia ya wananchi na wageni

waliohudhuria uzinduzi wa mradi huo uliofanyika katika kijiji cha Taif, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba kuwa, Mradi huo ni miongoni mwa hatua za utekelezaji wa ahadi zake kwa wananchi alizozitoa wakati akiomba ridhaa yao kuongoza Zanzibar katika uchaguzi wa mwaka 2010 kupitia mipango mbalimbali ya maendeleo.

Pamoja na kuwashukuru washirika wa maendeleo na taasisi nyingine pamoja na watu binafsi kwa mchango wao mkubwa katika kusaidia miradi ya maji nchini lakini alieleza"anaona faraja kwamba mambo mengi tuliyowaahidi wananchi katika mwaka 2010 tunayakamilisha. Tulipoahidi tulijua ahadi ni deni"



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimtwisha ndoo ya maji Bi. Mwajuma Ahmed Abdalla baada ya kufungua Mradi wa Maji safi na Salama katika kijiji cha Taif Wete Pemba Mkoa wa Kaskazini akiwa katika ziara ya kuifungua miradi mbalimbali ya Maendeleo tarehe 25 Agosti 2015. Mradi huu umefadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika AFDB,

## Uzinduzi wa barabara ya Wete – Gando na Wete Konde



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikata utepe kufungua Barabara ya Wete- Gando na Wete-Konde katika Mkoa wa Kaskazini Pemba katika ziara ya kuzindua miradi ya maendeleo katika Mkoa huo tarehe 27 Ogasti 2015. Kushoto ni Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu Issa Haji Ussi

Uzinduzi wa barabara za Wete- Gando na Wete- Konde ni muendelezo wa jitihada za Serikali ya Awamu ya Saba ya kuimarisha miundombinu ya kiuchumi Unguja na Pemba.

Barabara hizo zinaongeza idadi za barabara zilizomalizika kujengwa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba katika awamu hii ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2010 - 2015 ambapo kwa mujibu wa Ilani hiyo katika kipindi cha miaka mitano ilielekeza Serikali kujenga barabara za kiwango cha lami zenye urefu wa kilomita 76.6 kisiwani Pemba.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifuatana na viongozi wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano mara baada ya uzinduzi rasmi wa Barabara ya Wete - Gando katika katika ziara ya kuzindua miradi ya maendeleo Mkoa wa Kaskazini Pemba tarehe 27 Ogasti, 2015

Ni vyema kuwakumbusha wasomaji kuwa mwezi Machi 2014, Mheshimiwa Rais alizindua barabara za vijijini katika mkoa wa Kaskazini Pemba ambazo ni kutoka Kipangani hadi Kangagani ambayo inajulikana kama barabara ya Kangagani yenye urefu wa kilomita 2.7. Barabara nyingine ni ya Kojani yenye urefu wa kilomita 1.9 ambayo imeanzia kijiji cha Chwale hadi Likoni kwenda kisiwa cha Kojani, nyingine ni ya Pandani. Hii ina urefu wa kilomita 7.9 ambayo inaanzia kijiji cha Mzambarau Takao kupitia vijiji vya Pandani hadi Finya.

Barabara nyingine ni ya Mapofu ambayo imeanzia Mzambarau Karim kupitia Finya hadi kijiji cha Mapofu ambayo ina urefu wa kilomita 8.9. Nyingine ni barabara ya Daya yenye urefu wa kilomita 6.9 ambayo imeanzia kijiji cha Bahanasa hadi Daya na mwisho ni barabara ya Mtambwe yenye urefu wa kilomita 7.1 inayoanzia kijiji cha Makoongeni kupitia kijiji cha Daya hadi Mtambwe.

Ni jambo la kutia moyo na kujivunia kuona kuwa pamoja na kumalizika kwa barabara hizo, Serikali bado inaendelea na mpango wake wa ujenzi wa barabara nyingine katika mkoa huo ambazo ni barabara ya zamani ya kutoka Wete hadi Chake-Chake yenye kilomita 22.1 na pia inaifanyia marekebisho makubwa barabara ya Ole hadi Konde kuimarisha uwezo wake.

Kwa upande mwingine Serikali imeanza ujenzi wa barabara ya Ole hadi Kengeja (35 km). Barabara hii inaelezwa kuwa ilibuniwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar Mzee Abeid Amani Karume kwa hivyo ujenzi wake utatimiza ndoto ya mwasisi huyo ambaye alifariki kabla ya ndoto yake kutimia.

Katika hotuba yake kwa wananchi wakati wa uzinduzi wa barabara hizo uliofanyika katika kijiji cha Ukunjwi Wilaya ya Wete, Dk. Shein hakusita kuwakumbusha wananchi kuhusu matumizi bora ya barabara pamoja na kutumia fursa za kuwepo barabara hizo kuchangamkia fursa za kiuchumi kama vile kuongeza kilimo cha mbogamboga na matunda.

Ni ukweli usiofichika kuwa barabara hizo zimejengwa kwa gharama kubwa na fedha nyingine ni mikopo na misaada hivyo tunaungana na wito wa Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa kuwataka kuzitunza barabara hizo na kuwatahadharisha wananchi hao dhidi ya kukaidi amri ya serikali ya kutojenga katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara.

Dk. Shein alitumia fursa hiyo kuushukuru uongozi wa Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi ya Afrika (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (Saud Fund) kwa kusaidia ujenzi wa barabara hiyo.

## Kuweka Jiwe la Msingi la Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifungua pazia kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi la Hospitali mpya ya Abdalla Mzee iliyopo Mkoani Pemba akiwa katika ziara ya kufungua miradi ya maendeleo kisiwani Pemba tarehe 28 Ogasti, 2015

Hospitali ya Abdallah Mzee iliyoko Mkoani, mkoa wa Kusini Pemba ni moja ya hospitali za zamani kisiwani humo na tangu kuanzishwa kwake imejipatia sifa kubwa kutokana na kuwa kama ndio hospitali ya rufaa kisiwani Pemba.

Jambo moja ambalo liliifanya hospitali hiyo kuwa mashuhuri kisiwani humo ni kuwepo kwa madaktari bingwa kutoka Jamhuri ya Watu wa China kama ilivyo kwa hospitali kuu ya Mnazi Mmoja Unguja.

Hospitali hii hivi sasa inajengwa upya kwa msaada kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ili kuifanya iwe ya kisasa ikiwa ni sehemu ya mkakati wa serikali wa kuimarisha huduma za afya nchini.

Siku ya tarehe 27 Agosti, 2015 ilikuwa siku ya pekee iliyojaa furaha kwa wananchi wa Mkoani Pemba kwa kuwa walishuhudia sherehe za kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa hospitali hiyo mgeni rasmi akiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein.

Kwa mujibu wa taarifa ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dk. Mohamed Saleh Jidawi, itakapokamilika mwezi Septemba 2016, pamoja na uwezo wa kulaza wagonjwa 160, hospitali hiyo itakuwa na vifaa vyote muhimu vya kisasa vya uchunguzi wa maradhi.

Aidha, hospitali hiyo itakuwa na jengo la utawala, jengo la kupokelea wagonjwa, sehemu za kufulia, chumba cha kuhifadhia maiti, jiko na sehemu ya kuchomea taka.

Wakati serikali ya Jamhuri ya Watu wa China itatoa vifaa vyote vya hospitali hiyo kwa upande wake katika kuhakikisha hospitali inafikia viwango vya kimataifa, Mhe Rais aliahidi kuwa serikali ya Zanzibar itaweka mashine ya kisasa kabisa katika uchunguzi wa maradhi iitwayo Megnatic Renascence Imaging (MRI).

Katika hotuba yake kwenye hafla hiyo, Dk. Shein aliusifu urafiki na udugu wa wananchi wa Jamhuri ya Watu wa China na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwashukuru viongozi na wananchi wa China kwa namna wanavyowaunga mkono wananchi wa Zanzibar katika harakati zao za kujiletea maendeleo ikiwemo msaada wa ujenzi wa hospitali hiyo.

“hawa (wachina) ni marafiki zetu wa kweli kwani akufaaye kwa dhiki ndie rafiki” Dk. Shein aliwaeleza wananchi na viongozi waliohudhuria hafla hiyo huku akitoa shukrani maalum kwa Rais wa Jamhuri ya Watu wa China Xi Jinping kwa kuendeleza urafiki na udugu huo.

Katika salamu zake kwa wananchi kwenye hafla hiyo, Balozi Mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China nchini Mheshimiwa Xie Yunliang alieleza kuwa ujenzi wa hospitali hiyo ni uthibitisho mwingine wa udugu na urafiki wa watu wa China na Zanzibar uliodumu kwa miaka mingi.

“China inathamini sana udugu na urafiki wetu na Zanzibar na dhamira yetu kila siku ni kuona urafiki na udugu wetu unaimarika mwaka hadi mwaka kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili”alieleza Balozi Yunliang.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia ramani ya jengo la Hospitali mpya ya Abdalla Mzee iliyopo Mkoani Pemba itakavyokuwa baada ya ujenzi kukamilika akiwa katika ziara ya kufungua miradi ya maendeleo kisiwani Pemba tarehe 28 Ogasti, 2015

Kwa hakika ujenzi wa hospitali hii kunaendeleza historia ya miaka 51 ya ushirikiano katika sekta ya afya kati ya Zanzibar na China. Historia inaonesha mwaka mmoja baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China iliipa msaada mkubwa Zanzibar kwa kuleta timu ya madaktari bingwa ambapo chini ya utaratibu huo hadi sasa imefikia timu ya 31 ya madaktari hao.

## Uzinduzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akielekeza matumizi ya asili ya pakacha katika uchumaji wa karafuu mbele ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili katika banda la maonesho ya bidhaa za karafuu. Maonesho hayo yalifanyika katika kiwanda cha Makonyo Wawi Wilaya ya Chechake Pemba tarehe 26 Ogasti, 2015

Moja kati ya tukio kubwa na la kihistoria lililofanyika wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais kisiwani Pemba hivi karibuni ni uzinduzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu.

Uzinduzi wa mfuko huo ni hatua nyingine muhimu ya kuendeleza zao hilo na kuzifanya jitihada za serikali za kuimarisha zao la karafuu kuwa endelevu na lenye kuleta tija kwa washiriki wote hususan wakulima kwa upande mmoja na kurejesha hadhi ya zao hilo na hatimae kuchukua nafasi yake katika uchumi wa Zanzibar.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia koja la karafuu katika moja ya banda la maonesho ya bidhaa za karafuu. Maonesho hayo yalifanyika katika kiwanda cha Makonyo Wawi Wilaya ya Chechake Pemba tarehe 26 Ogasti, 2015

Kwa hakika hatua ya Serikali ya Awamu ya Saba chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kulifufua zao la karafuu ni jambo linalopaswa kupongezwa na kushukuriwa kwa kila wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba.

Kudorora kwa zao la karafuu hadi kufikia mikarafuu kuonekana si chochote si lolote na kuwafanya wakulima wa zao hilo kuyakimbia mashamba yao hadi sasa shamba la mikarafuu kuonekana mali kama mgodi wa dhahabu sio tu ni jambo la kujivunia bali ni uthibitisho wa dhamira ya kweli ya uongozi wa Awamu ya Saba kuimarisha zao hilo.

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais mpango wa kufufua zao la karafuu ni utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015 iliyoahidi kuimarisha zao la karafuu bila ya kulibinafsisha tofauti na Ilani za baadhi ya vyama vingine vilivyojiegemeza katika ubinafsishaji wa zao hilo.

Kwa hakika ni jambo la kutia moyo na faraja kubwa kwa kila mwananchi na kila kiongozi wa serikali ya Awamu ya Saba anaposikia taarifa kuwa wakulima wa karafuu katika misimu mine iliyopita wamejipatia jumla ya shilingi bilioni 231.2 kutoka shilingi bilioni 42.6 miaka mitano kabla ya hapo ikiwa ni ongezeko la asilimia 359.4.

Haya ni mafanikio makubwa na ya kujivunia kwa uongozi wa Awamu ya Saba kwa kuwa umeonesha njia bora ya kuwatumikia wananchi. Uongozi umedhihirisha kuwa uko kwa ajili ya wananchi na kwa faida ya wananchi.

Haihitaji mtaalamu wa uchumi aliyebobea kutafsiri matokeo ya fedha hizo kuwemo katika mifuko ya wananchi. Hii ni moja ya kumbukumbu za serikali ya Awamu ya Saba itakayodumu kwa miongo mingi miongoni mwa wakulima wa karafuu na wananchi wa Zanzibar.

Sherehe za uzinduzi wa Mfuko huo ambazo zilifanyika katika viwanja vya kiwanda cha Makonyo, kilichoko Wawi Chake Chake Pemba zilifana sana sio tu kwa sababu ziliwakusanya karibu washirika wote wa zao la karafuu ndani na nje ya nchi lakini pia maonesho ya zao hilo kuanzia utafiti wa udongo, aina ya vitalu, uvunaji, uanikaji hadi karafuu kumfikia mteja yaliandaliwa vyema.

Sherehe zilipambwa na matukio mbalimbali yakiwemo ya utoaji vyeti kwa wakulima bora na wauzaji bora wa zao hilo, wageni mashuhuri wa ndani na nje ya nje kutambulishwa na kupata fursa ya kusalimiana na mgeni rasmi.

Yote haya yalifanyika kuthibitisha kile alichokieleza Mheshimiwa Rais katika hotuba yake akiuzindua mfuko huo kuwa "kazi ya karafuu si ya mtu mmoja bali ni ya ushirikiano na washirika wengi wakiwemo wakulima, Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) pamoja na wafanyabiashara wa ndani na nje"

Ni lazima kuipongeza Serikali kwa kuanzisha mfuko huu ambao tayari manufaa yake yameonekana miongoni mwao ni hundi ya shilingi milioni 60 iliyotolewa wakati wa uzinduzi ikiwa ni malipo

ya bima kwa wakulima wa karafuu watakaoanguka mikarafuu wakati wa kuchuma zao hilo.

Misaada ya kila aina kwa wakulima ukiwemo ulinzi wa maisha yao kupitia bima ya ajali, mikopo isiyo na riba, upatikanaji wa vifaa vya kuchumia na kuanikia karafuu pamoja na vituo vya kuuzia karafuu vyenye huduma nzuri ikiwa ni tafsiri ya vitendo ya lugha ya biashara ya siku hizi kuwa 'mteja ni mfalme' yote haya ni katika kutekeleza dhamira ya serikali ya kulifanya zao la karafuu kuwa ni zao muhimu na linabaki kuwa utambulisho wa Zanzibar.

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais "wakulima sasa wana matumaini makubwa na Mfuko huo" kwa kuwa wanaamini kuwa ni chombo chao muhimu katika kuendeleza zao hilo na kusisitiza kuzingatiwa masharti ya mfuko katika utendaji lakini hata hivyo tunapaswa kuwakumbusha wakulima wetu maneno ya wahenga kuwa 'abwebwae hujikaza' ili wasibweteke!



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia karafuu zilizokuwa katika daraja la kwanza zikiwa katika majamvi ambazo zinakauka kutokana na hali nzuri ya hewa wakati wa Uzinduzi wa Mfuko wa wa Maendeleo ya Zao la Karafuu, Utambulisho Maalum wa Karafuu Zanzibar na Matumizi mazuri ya Tasnia ya Malibunifu katika kiwanda cha Makonyo Wawi Wilaya ya Chechake Pemba tarehe 26 Ogasti, 2015

# Uzinduzi wa Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Asili na Mazingira



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Afisa Misitu Asili Jamii Bi. Rahika Hamad Suleiman kuhusu utumiaji wa majiko kwa makaa nafuu na gesi, alipotembelea maonesho ya kazi mbali mbali katika uzinduzi wa Mradi wa (HIMA) katika hifadhi ya Misitu asili kituo cha Jamii Makangale ndani ya Msitu wa Ngezi Mkoa wa Kaskazini Pemba tarehe 26 Ogasti, 2015

Ni mwendo wa karibu dakika 40 kutoka mji wa Chake-Chake hadi katikati ya msitu wa Ngezi ulioko Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba. Msitu huo ni kati ya misitu miwili mikubwa Zanzibar- mwingine ukiwa ni Jozani. Msitu huu kama ulivyo msitu wa Jozani, ni maarufu ulimwenguni hasa kwa watafiti wa masuala ya viumbehai kwa kuwa msitu huu umesheheni hazina kubwa ya baianuai.

Kwenye kijiji cha Makangale pembeni tu mwa msitu huo kuna kila aina ya shamrashamra za wananchi wengi wenye furaha na nyuso zilizojaa matumaini wakiwa na wageni mbalimbali kutoka sehemu nyingine za visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na wageni wengine kutoka Tanzania Bara-wote wakiwa wadau wa masuala ya mazingira.

Wote hao wakimsubiri mgeni rasmi Rais wa Zanzibar

na Mwenyekti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika sherehe hizo. Tofauti na sherehe nyingine, hii ni sherehe ya aina yake na inafanyika katika eneo la aina yake pembeni ya -katikati ya msitu.

Ni sherehe ya uzinduzi wa mafanikio ya mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Asili (HIMA). Katika eneo la sherehe katikati ya msitu huo kuna maonesho ya kazi mbalimbali zinazofanywa na vikundi vya wanamazingira (zikiwemo za ujasiriamali)-washiriki wa programu za HIMA ambazo zinaambatana na malengo ya mradi huo.

Msitu wa Ngezi upo karibu na bahari pamoja na misitu mingine, hivyo kwa pamoja inakuwa miongoni mwa misitu ya pwani ya Afrika Mashariki ambayo ni moja ya sehemu muhimu za baianuai muhimu 200 za kidunia.

Mradi wa HIMA ambao ulitekelezwa kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka 2014 lengo lake lilikuwa ni kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa kutokana na ukataji wa miti na uharibifu wa misitu huku ukiwanufaisha wananchi kutokana na juhudi zao za kuhifadhi misitu ya asili ambayo ina mchango mkubwa katika kupunguza hewa ukaa. Kwa maelezo mengine lengo hilo la mradi wa HIMA linakwenda sambamba utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Ukataji Miti ovyo na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMU)

Chini ya mradi huo wananchi wameweza kupata elimu na uzoefu wa kutengeneza majiko sanifu na matumizi bora ya nishati mbadala ya gesi, ufugaji wa nyuki, kufanya tafiti mbali mbali za mali asili pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Ndio maana katika hotuba yake kwenye sherehe hizo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein mbali ya kuipongeza na kuishukuru serikali ya Norway na Shirika la CARE International lililosimamia mradi huo, alitambua umuhimu wa mradi huo na mchango wake mkubwa sio katika hifadhi ya misitu ya asili pekee lakini pia katika kuimarisha harakati za ujasiariamali katika maeneo ya mradi.

Hii ni sehemu ya jitihada za kimataifa za kukabiliana na matatizo ya kimazingira yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo sasa ni miongoni mwa ajenda kuu za mazingatio katika masuala ya kimataifa.

Kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa hivi karibuni, Zanzibar ina jumla ya maeneo 148 ambayo yanaingia maji ya chumvi kwa sababu ya kupanda kwa kina cha bahari kulikosababishwa na mabadiliko ya tabianchi pamoja na ukatwaji wa mikoko. Kati ya maeneo hayo, 123 yapo Pemba na 25 Unguja.

Ni jambo la kutia moyo kuona dhana ya uhifadhi shirikishi kama hii ya mradi wa HIMA imepokelewa vyema na wananchi. Hivi sasa wananchi wanatambua wajibu wa kuhifadhi misitu ya asili kwa kuzingatia manufaa wanayoyapata katika kutekeleza wajibu wao huo.

Miongoni mwa faida walizopata ni pamoja na kuweza kupanda miti zaidi ya milioni 5.35 katika mashamba yao binafsi, kuanzisha kilimo cha mbogamboga, wamepatiwa taaluma ya ufugaji nyuki na kupewa vifaa vyake, wamefundishwa kutengeneza majiko sanifu, wamepatiwa mafunzo ya upimaji wa hewa ukaa, ajira na zaidi wamepatiwa jumla ya shilingi milioni 459 kama motisha ya kuhifadhi misitu.

Chini ya mradi wa HIMA, tafiti mbalimbali zilifanywa zinazohusiana na utekelezaji wa malengo ya mradi ikiwemo sensa ya miti iliyofanyika mwaka 2013. Matokeo ya sensa hiyo yametoa taswira halisi ya rasilimali ya miti hapa nchini ikiwemo ya misitu, miti na mimea ya matunda na viungo ikiwemo mikarafuu.

Katika mnasaba huo Dk. Shein mbali ya kueleza kufurahishwa kwake na matokeo ya tafiti hizo, aliipongeza Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kukamilisha tafiti mbali mbali kupitia mradi wa HIMA kwa mafanikio makubwa na kuuhimiza uongozi wa Wizara hiyo kutunza na kutumia matokeo ya tafiti hizo ambazo zinakadiriwa kufikia 20 na kuzitaka Idara nyengine za Serikali kufuata mfano wa wizara hiyo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na Mwakilishi wa Shirika la Kimataifa la Care Tanzania Bw. Paul Daniel (katikati) wakati alipowasili katika sherehe za Uzinduzi wa Mradi wa (HIMA) katika hifadhi ya Misitu asili kituo cha Jamii Makangale ndani ya Msitu wa Ngezi Mkoa wa Kaskazini Pemba tarehe 26 Ogasti, 2015. Kulia ni Balozi wa Norway Bw. Trygve Bendiksby

# Matayarisho ya Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri yamekamilika

Hivi karibuni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alifanya ziara fupi kutembelea eneo ambalo linatarajiwa kujengwa Bandari mpya ya Mpigaduri.

Kwa nchi za visiwa kama Zanzibar bandari ni njia pekee kuu ya kusafirishia mizigo kutoka na kuingia iwe ya biashara au matumizi mengine na hivyo kuifanya kuwa na umuhimu wa kipekee kwa uchumi na maendeleo yake.

Kwa hivyo taarifa za kuwa maandalizi ya ujenzi wa bandari Mpigaduri kuwa yamekamilika zimepokelewa kwa furaha kubwa si kwa viongozi wa serikali pekee bali hata kwa wananchi wengi waliokuwa wakisubiri kwa miaka mingi wakielewa kuwa ujenzi wa bandari hiyo unaleta matumaini mapya kwa maendeleo yao na maendeleo ya Zanzibar kwa jumla.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara hiyo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alisema azma ya kujenga bandari hiyo ilikuwepo tangu uongozi wa Awamu ya Tano chini ya Rais Dk. Salmin Amour lakini uwezo wa kupata fedha za kutekeleza mradi huo umepatikana katika awamu ya saba baada ya mazungumzo ya mara mbili kati ya Rais Dk. Ali Mohamed Shein na Rais wa Jamhuri ya watu wa China bwana Xi Jinping ambapo serikali ya China ilikubali kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo.

Wapo waliobeza na kusema mradi huo ni hadithi za alinacha lakini leo imekuwa tofauti kwani wahenga walisema 'penye nia pana njia' na kuongeza kuwa 'ukweli ukidhihiri uongo hujitenga'.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi Mkuu wa Shirika la Bandari Mbarouk Hamadi Mbarouk wakati alipotembelea Eneo la Ujenzi wa Bandari Mpya ya kisasa Mpigaduri Maruhubi Wilaya ya Mjini, tarehe 02 Disemba 2015. Bandari hiyo itajengwa na Kampuni ya China Harbour Engineering Company Ltd (CHEC)

Naam kweli imedhihiri, Serikali imeonesha ukweli wake katika jambo hili.

"Sisi awamu hii tumekwenda mbele zaidi, tumetafuta fedha na tumefanikiwa kutokana na urafiki wetu na serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambao wametupatia mkopo wa ujenzi wa bandari hii" Dk. Shein aliwaeleza waandishi wa habari kwa furaha.

Mradi wa ujenzi wa bandari ya Mpigaduri unatarajiwa kuanza Januari, 2016 ambapo kwa mujibu wa taarifa za wizara ya Miundombinu na Mawasiliano masuala yote muhimu ya utekelezaji wa mradi huo umekamilika na ithibati ya mkopo kutoka China imepatikana.

Kukamilika kwa mradi huo ni hatua muhimu katika kuirejesha Zanzibar kuwa kituo cha biashara Afrika Mashariki na hivyo kusaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la ajira nchini hasa kwa vijana.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ujenzi wa bandari hii utafanyika kwa awamu tatu tofauti kulingana na mahitaji ya wakati husika. Awamu ya kwanza ujenzi wake utafanywa na kampuni ya CHEC kutoka nchini China na utagharimu Dola za kimarekani milioni 231.4. Awamu hiyo inatarajiwa kukamilika ndani ya miaka mitatu kwa kujengwa bandari kamili yenye kila huduma zitakiwazo kwa bandari za kisasa na awamu nyingine zitatekelezwa kulingana na kuongezeka kwa mahitaji ya miaka ijayo.

Ni vyema kubainisha kuwa ujenzi wa bandari hii ni hatua nyingine muhimu ya kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi sambamba na kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii Zanzibar.

# ZSTC yatunukiwa tunzo na taasisi ya kimataifa

Imezoweleka miongoni mwa wananchi kwamba kauli na maandiko ya wanasiasa hasa wakati wa kampeni za kuomba kura, mara nyingi huonekana kama ni mkakati unaotumiwa na wanasiasa kuomba kura kwa lengo la kuingia madarakani.

Dhana hiyo miongoni mwa wananchi imethibitishwa na baadhi ya viongozi katika baadhi ya majimbo, ambako viongozi waliochaguliwa na wananchi wamehama kwenye majimbo yao mara tu baada ya kuchaguliwa.

Lakini hali haiko hivyo kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, ambaye alionekana na bado anaendelea kuonekana kuwa mkweli kutokana na kutekeleza asilimia kubwa ya yale aliyoyaahidi kwa wananchi wakati alipokuwa akiomba kura katika uchaguzi mkuu wa 2010. Miongoni mwa mambo mengi aliyoyaahidi ni kuliimarisha zao la karafuu ambalo lilishapoteza hadhi yake.

Miaka mitano baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa kuanza kutekeleza azma yake ya kuliimarisha zao la karafuu, Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) Bibi Mwanahija Almasi Ali alieleza kuwa Shirika lake limepata mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu yake hadi kufikia kutambuliwa kimataifa.

"Tumetunukiwa tunzo ya kimataifa iliyoambatana na cheti kutoka taasisi ya kimataifa ya Global Trade Leaders Club ya Hispania, kutokana na utendaji wa shirika, utoaji wa bidhaa bora na huduma nzuri zinazotolewa na shirika" alieleza Bi Mwanahija.



Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la ZSTC Bi. Mwanahija Almasi Ali akiwa ameshika tunzo maalumu ya kimataifa iliyozawadiwa Shirika la ZSTC kutoka kwa taasisi ya 'Global Trade Leaders Club'ya Hispania inayolitambua Shirika kwa utoaji wa bidhaa bora na huduma nzuri.

Mkurugenzi huyo Mwendeshaji aliyasema hayo wakati alipokuwa akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Mfuko wa Kuendeleza Karafuu shughuli ambayo pia ni hatua nyengine ya kuliendeleza zao hilo kwa kuliwekea mipango endelevu.

Mafanikio hayo yanatokana na dhamira ya kweli ya Serikali katika utekelezaji wa mkakati maalum uliopangwa wa kuimarisha zao la karafuu ndani ya kipindi cha miaka 10 ili kuhakikisha kuwa zao hilo linaendelea kuwa ni shemu muhimu kwa uchumi na maisha ya watu wa Zanzibar.

Miongoni mwa malengo yaliyokuwa yamepangwa kutekelezwa ni kutafuta masoko ya uhakika, kuitunza mikarafuu iliyopo pamoja na kupanda mikarafuu mingine mipya.

Baada ya kukamilisha utafiti wa soko la karafuu, Serikali ilifikia maamuzi ya kupandisha bei ya zao hilo kwa wakulima kutoka TZS 5,000 mwaka 2010 hadi kufikia 14,000, kwa kilo moja, sawa na ongezeko la asilimia 180. Katika bei hiyo Serikali iliamua kumpa mkulima asilimia 80 na Serikali inachukua asilimia 20 ambazo kwa kiasi kikubwa zinatumika kuimarisha uzalishaji wa karafuu.

Ingawa uamuzi huo ulihitaji moyo kuutekeleza kutokana na ukweli kwamba bei ya karafuu kwenye soko la dunia inakuwa haitulii, Serikali imeweza kuidumisha bei hiyo tokea ilipopandishwa licha ya bei ya karafuu kupanda na kushuka katika soko la dunia.

Katika kipindi cha 2010 – 2014, jumla ya miche ya mikarafuu milioni 3.7 iligaiwa kwa wakulima Unguja na Pemba. Tafiti zilizofanywa zimebainisha kuwa wastani wa asilimia 44 ya miche hiyo imeota na inaendelea kunawiri vizuri hivi sasa.

Hayo ni mafanikio makubwa ya kujivunia katika zao la karafuu hasa ikizingatiwa kwamba kabla ya hatua hiyo mashamba ya mikarafuu yalikuwa yameachwa na kudharauliwa kama vile yalikuwa hayana wenyewe. Mikarafuu mingi ilikufa kwa kukosa kushughulikiwa. Wako wananchi waliothubutu kuvunja sheria kwa kuikata kwa ajili ya kuchoma makaa. Mikarafuu ilipunguwa kwa wingi sana katika sehemu zote za Unguja na Pemba.

Kwa lengo la kurahisisha upangaji na utekelezaji wa mipango na kujenga mwelekeo sahihi, Serikali iliamua kuihesabu mikarafuu iliyopo Uguja na Pemba kupitia tathmini ya sensa ya miti (Woody Biomass Survey) iliyofanywa mwaka 2013. Kupitia Sensa hiyo, ilibainika kuwa Zanzibar ilikuwa na idadi ya Mikarafuu 4,131,783 mwaka huo, ambapo Unguja ilikuwa na mikarafuu 277,197 na Pemba ilikuwa na mikarafuu 3,854,587. Idadi hiyo imeongozeka hivi sasa kutokana na mikarafuu iliyopandwa baada ya kipindi hicho cha mwaka 2013.

Vile vile, katika sensa hiyo ilibainika kuwa asilimia 60 ya mikarafuu iliyokuwepo ilikuwa ni midogo yenye umri kati ya mwaka mmoja hadi sita. Tafsiri ya takwimu hizo ni kuwa, bado kuna nafasi kubwa ya kuongeza uzalishaji wa karafuu kwa wingi zaidi kwa siku zijazo wakati mikarafuu hiyo itakapoanza kuzaa ikiwemo hii inayoendelea kupandwa kila mwaka.

Katika jitihada za kuimarisha taaluma na maarifa ya wakulima juu ya zao la karafuu, Serikali lianzisha utaratibu wa kutoa mafunzo ya ukulima wa karafuu kupitia shamba darasa. Kupitia mpango huo wakulima wamejitokeza kwa wingi katika darasa hizi na zimesaidia sana katika kufanikisha uzalishaji wa miche, upandaji, utunzaji wa mashamba na hifadhi ya mazingira.

Ili kuwaondoshea wakulima usumbufu waliokuwa wakiupata wakati wa kuuza karafuu, Serikali imefanya jitihada kubwa katika kipindi hiki cha miaka mitano za kuimarisha vituo vya kuuzia karafuu kwa kuvifanyia matengenezo makubwa vituo vya zamani na kujenga vipya karibu na maeneo yote yanayozalishwa karafuu. Katika vituo hivyo, Serikali imehakikisha upatikanaji wa huduma zote muhimu unaimarishwa.

Kwa upande mwengine, Serikali ilitambua kuwa pamoja na juhudi zote hizo, zao la karafuu lingeweza kuathiriwa vibaya kutokana na magendo ya karafuu na hivyo kulazimika kuchukua hatua madhubuti katika kuzuwia na kupambana na magendo ya karafuu. Hivyo Serikali ilipanga mikakati imara ambayo kwa kipindi hiki cha miaka mitano imeleta mafaniko makubwa. Kwa kiasi kikubwa Serikali imeweza kupunguza magendo ya karafuu na kimsingi hivi sasa imekuwa fahari kwa wakulima wa karafuu kuuza karafuu zao katika vituo vya ZSTC.

Kwa upande mwengine, Serikali ililazimika kuchukua maamuzi mazito ya kulifanyia mageuzi Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ili kulipa nguvu katika shughuli za ununuzi, usafirishaji, uuzaji na utafutaji wa masoko nje ya nchi. Shirika lilipewa nguvu kiutendaji na kiutawala, limeajiri wafanyakazi wenye ujuzi na utaalamu ili kuliongoza shirika hilo kitaalamu zaidi na kulipa mwelekeo wa kibiashara.

"Leo hii sote tunajivunia kuona namna Shirika lilivyonawiri na kutononoka. Limekuwa na ubunifu na ujasiri wa kibiashara na linaenda likiwa na mashirikiano mazuri na uongozi wa juu wa Wizara. Mashirikiano haya mazuri ndiyo yaliyotuwezesha kuzindua mfuko huu wa maendeleo ya karafuu ambayo ni hatua nyengine ya maendeleo katika jitihada zetu za kuimarisha zao hili". Alisema Dk. Ali Mohamed Shein katika sherehe za uzinduzi wa mfuko wa karafuu.

"Nashukuru kuona juhudi tulizochukua kwa mashirikiano makubwa katika mambo hayo muhimu zimetuwezesha kuongeza uzalishaji wa zao hili kutoka tani 2,673 katika mwaka nilioingia madarakani, 2010 hadi kufikia tani 5,340 mwaka 2014. Mafanikio tuliyoyapata katika kulifufua zao hili ni matokeo ya upangaji na utekelezaji wa mipango mingi tukiwa na mashirikiano makubwa". Aliongeza.

